ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 23*** ***29th April, 2022***

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*To The Gazette Of The United Republic Of Tanzania No. 23 Vol. 103 Dated 29th April, 2022*
Printed By The Government Printer, Dodoma By Order Of Government

TANGAZO LA SERIKALI Na. 259 la tarehe 29/4/2022

SHERIA YA TAKWIMU (SURA YA 351)

# AMRI

*(Imetungwa chini ya kifungu cha 21)*

SHERIA YA TAKWIMU (SENSA YA WATU NA MAKAZI) AMRI, YA MWAKA 2022

KWA KUWA, kifungu cha 21 cha Sheria ya Takwimu, kinampa mamlaka Rais, kwa Amri ya maandishi, kuelekeza kwamba Sensa ya Watu na Makazi ifanyike nchi nzima au sehemu yoyote ya nchi;

NA KWA KUWA, katika kuandaa Sensa, Amri itaainisha tarehe ambayo Sensa ya Watu na Makazi itafanyika, taarifa za kidemografia, hali ya ulemavu, uhamiaji, vitambulisho vya utaifa na uhai wa wazazi, elimu, shughuli za kiuchumi, umiliki wa ardhi na TEHAMA, hali ya uzazi, vifo na vifo vitokanavyo na uzazi katika kaya, hali ya umiliki wa nyumba, vifaa/rasilimali na udhibiti wa mazingira, kilimo, mifugo uvuvi na misitu, huduma za kijamii, majengo na anwani za makazi;

NA KWA KUWA, ninaridhika kwamba Amri hii chini ya kifungu cha 21 cha Sheria ya Takwimu, ni muhimu kuandaa Sensa ya Watu na Makazi kwa ajili ya kuleta maendeleo katika nyanja mbalimbali nchini;

KWA HIYO BASI, MIMI, SAMIA SULUHU HASSAN, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika utekelezaji wa Mamlaka niliyopewa chini ya kifungu cha 21 cha Sheria ya Takwimu, ninatoa Amri ifuatayo:

Jina

1. Amri hii itaitwa sheria ya takwimu (sensa ya watu na makazi) amri, ya mwaka 2022.

Kutumika

2. Inaelekezwa kwamba Sensa ya Watu na Makazi itafanyika kuanzia tarehe 23 Agosti hadi tarehe 30 Septemba, 2022.

Muda wa kufanya sensa

3.-(1) Kwa kuzingatia aya ndogo ya (2), zoczi la kuhesabu watu katika Sensa ya Watu na Makazi litafanyika kila siku kuanzia saa kumi na mbili Alfajiri mpaka saa moja jioni.

(2) Zoezi la kuhesabu watu katika Sensa ya Watu na Makazi kwa usiku wa kuamkia siku ya Sensa ya tarehe 23 Agosti liataanza saa sita na dakika moja usiku.

4. Katika kukusanya taarifa kwa ajili ya Sensa, Karani wa Sensa-

(a) atakuwa na kitambulisho;

(b) Atapita kaya zote pamoja na vituo vyote vinavyotoa huduma mbalimbali za kijamii;

(c) atatumia kishikwambi; na

(d) ataambatana na wenyeviti wa Serikali za Mitaa/Vijiji/Sheria wa maeneo husika.

Dodoma
21 Machi, 2022

SAMIA SULUHU HASSAN
*Rais*